# Ruwaza ya Viambishi vya Nafsi na Njeo katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa

*Maisha Laston Mwaipaja*[1] na *Elither Vincent Kindole*[2]
[1]*Shule ya Sekondari Kanda, Rukwa*
[2]*Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

**Ikisiri**

**Makala haya yamechunguza ruwaza ya viambishi vya nafsi na njeo katika vitenzi vya lugha ya Kifipa[1] kwa kuongozwa na Nadharia Akisi ya Baker. Data za makala haya zilipatikana kwa mbinu za hojaji na usaili ambapo vitenzi sabini na vitano (75) vya Kiswahili vilitafsiriwa kwa Kifipa na baada ya kutafsiriwa watoataarifa waliombwa wavitamke taratibu kwa Kifipa. Data zilizopatikana zilichanganuliwa kwa mkabala wa kitaamuli na kuwasilishwa kwa majedwali na vielelezo mbalimbali. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa, lugha ya Kifipa ina nafsi tatu zenye umoja na wingi. Nafsi ya kwanza umoja na nafsi ya tatu umoja huwakilishwa na viambishi viwiliviwili kwa kila nafsi. Nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili umoja na wingi na nafsi ya tatu wingi huwakilishwa na kiambishi kimojakimoja kwa kila nafsi. Viambishi vyote vya nafsi hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi. Kwa upande wa njeo, lugha ya Kifipa ina njeo tatu; wakati uliopita, uliopo na ujao. Wakati uliopita na uliopo zina viambishi bayana ilhali wakati ujao huamriwa na masuala ya kifonolojia kwa kutumia umbo la kitenzi cha wakati uliopo. Wakati uliopita una viambishi viwili vinavyotokea kwa pamoja kwenye kitenzi. Kiambishi kimoja cha wakati uliopita hutokea kabla ya mzizi na kingine hutokea baada ya mzizi wa kitenzi. Kiambishi cha wakati uliopo hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi.**

**Maneno Muhimu:** *Viambishi, Nafsi, Njeo, Mzizi, Ruwaza.*

**Utangulizi**

Ruwaza ni utaratibu unaopaswa kuzingatiwa katika kufanya au kuchunguza jambo. Massamba (2004) anaeleza ruwaza kuwa ni utaratibu wa kimpangilio wa vipashio vya lugha. Vipashio vya lugha vipo vya kisemantiki, kisintaksia, kifonolojia na kimofolojia. Vipashio vinavyorejelewa kwenye makala haya ni vipashio vya kimofolojia ambavyo ni viambishi vya nafsi na njeo kwenye vitenzi vya lugha ya Kifipa. Wanaisimu wengi wamechunguza ruwaza ya viambishi vya nafsi na njeo kwenye lugha mbalimbali za Kibantu. Matokeo ya tafiti zao yamegawanyika kwenye makundi mawili. Kundi la kwanza linadai kuwa kiambishi cha nafsi hutokea kwanza kisha hufuatiwa na viambishi vingine (Rubanza, 1996; Wesana-Chomi, 2003; Habwe na Karanja 2004; Massamba, 2004; Kihore, Massamba na Msanjila, 2009; Mgullu, 2010). Kundi la pili linaeleza kuwa viambishi vya nafsi na njeo vinaweza kubadilishana nafasi ya kutokea ambapo kuna mazingira kiambishi cha nafsi kinaweza kutangulia na kinyume chake (Lusekelo, 2007; Nyinondi, 2013; Charwi, 2019). Kutofautiana huko kwa wataalamu ndiko kulikotupa shauku ya kitaaluma kuchunguza hali ilivyo kwenye lugha ya Kifipa. Hii ni kwa sababu kuna uwezekano wa kuwa na ruwaza zaidi ya zilizobainishwa endapo tafiti zaidi zitafanywa kwenye lugha mbalimbali za Kibantu. Jambo hilo litatuongezea maarifa na kuepusha mahitimisho ya jumla kuhusu ruwaza ya viambishi vya nafsi na njeo katika lugha za Kibantu.

Vifupisho na misimbo mbalimbali imetumika katika uandishi wa makala haya. Vifupisho na misimbo hiyo ni kama ifuatayo; **NABA** (Nadharia Akisi ya Baker), **Mzz** (Mzizi), **Nfs** (Nafsi), **NfsIu** (Nafsi ya kwanza umoja), **NfsIw** (Nafsi ya kwanza wingi), **NfsIIu** (Nafsi ya pili umoja), **NfsIIw** (Nafsi ya pili wingi), **NfsIIIu** (Nafsi ya tatu umoja), **NfsIIIw** (Nafsi ya tatu wingi), **Nj** (Njeo), **Njwl**

[1] Kifipa ni lugha inayoongelewa na watu wanaoitwa Wafipa wanaoishi kwenye eneo la Ufipa, mkoani Rukwa, Kusini-Magharibi ya Tanzania baina ya ziwa Tanganyika na ziwa Rukwa (Batibo, 2010).

(Njeo ya wakati uliopita), **Njwp** (Njeo ya wakati uliopo), **Njwj** (Njeo ya wakati ujao), **Ii** (Irabu ishilizi), **:** (Wakaa).

**Nadharia Akisi ya Baker**

Nadharia hii iliasisiwa na Baker mwaka 1985 kupitia makala yake ya *"The Mirror Principle and Morphosyntactic Explanation"*. Kwa nyakati tofauti, Baker mwenyewe aliiendeleza nadharia yake mara mbili; mwaka 1988 na 2002. Nadharia hii inaeleza kuwa uambishaji au unyambulishaji wa kimofolojia ni lazima uakisi uambishaji au unyambulishaji wa kisintaksia na kinyume chake. Anaendelea kueleza kuwa endapo kitenzi kitapitia michakato miwili yaani uambishaji na unyambulishaji basi viambishi kama vile vya nafsi, njeo na hali hutokea karibu na mzizi wa kitenzi ama mbali kutokana na uhusiano wa kimaana na sarufi ya lugha husika. Baker (1985) alifafanua kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya michakato ya kimofolojia na kisintaksia licha ya kuwa mofolojia hujihusisha na maumbo ya maneno na namna yanavyohusiana na sintaksia ya sentensi inayohusika. Aliendelea kufafanua kuwa mpangilio wa kimofolojia hubainishwa na mfuatano wa viambishi ambao lazima ufanane na mfuatano wa viambishi kisintaksia wa lugha husika.

Katika maendeleo ya nadharia yake, mwaka 1988, Baker aliongeza ufafanuzi kuwa sintaksia hutenda kazi katika maneno na viambishi. Aliendelea kufafanua kuwa maneno changamani huundwa kwa kanuni za kisintaksia hususan mjongeo wa neno kuu ambapo mzizi leksika hugubikwa katika viambishi. Kama muundo wa kimofolojia wa maneno changamani unatokana na mjongeo wa neno kuu ambapo mzizi leksika hugubikwa na viambishi, basi kanuni akisi hufuata moja kwa moja (Baker, 1988). Pia, Baker (2002) aliongezea kuwa mfuatano wa viambishi katika maneno changamani ni lazima uakisi mchakato asilia wa kisintaksia unaowezesha neno kuu linaloshabihiana na viambishi hivyo kuambikwa katika utaratibu sahihi.

Nadharia hii inaegemezwa na misingi mitatu. Msingi wa kwanza unadai kuwa utokeaji wa viambishi unatawaliwa na kanuni za kimofolojia. Hii ina maana kwamba viambishi katika neno havitokei kiholela, bali kuna utaratibu maalumu unaoamua mpangilio wa kimofolojia wa utokeaji wa viambishi hivyo. Msingi huu pia unadai kuwa katika michakato ya uambishaji na unyambulishaji kuna baadhi ya viambishi hutokea karibu na mzizi wa kitenzi na vingine hutokea mbali na mzizi wa kitenzi kutokana na uhusiano wa kimaana na sarufi ya lugha husika. Msingi wa pili unadai kuwa unyambulishaji unatawaliwa na kanuni za kisintaksia ambazo viambishi nyambulishi lazima vizingatie. Hii ina maana kwamba vinyambulishi vinaweza kutokea zaidi ya viwili kwenye kitenzi kimoja kama vile kinyambulishi cha kauli ya kutendea na kutendewa. Katika muktadha huo kanuni za kisintaksia ndizo huamua kinyambulishi kipi kitokee kwanza na kipi kifuate. Msingi wa tatu unadai kuwa unyambulishaji kimofolojia ni lazima uakisi unyambulishaji kisintaksia na kinyume chake.

Katika makala haya tumetumia msingi mmoja unaodai kuwa utokeaji wa viambishi na mfuatano wake unatawaliwa na kanuni maalumu za kimofolojia. Vilevile msingi huu unadai kuwa katika mchakato wa uambishaji na unyambulishaji kuna baadhi ya viambishi hutokea mbali na mzizi wa kitenzi na vingine hutokea karibu kutokana na uhusiano wa kimaana na sarufi ya lugha husika. Msingi huu uliteuliwa kutokana na utafiti kukusudia kuchunguza ruwaza (maumbo na nafasi/utaratibu wa utokeaji) wa viambishi vya nafsi na njeo katika vitenzi vya lugha ya Kifipa ambavyo kimsingi havijitokezi kiholela, bali kuna kanuni maalumu za kimofolojia zinazoamua kiambishi kipi kitokee wapi, kipi kitangulie kutokea na kipi kifuate. Hivyo basi, msingi huu wakati wa uchanganuzi wa data, ulituwezesha kubainisha na kufafanua ruwaza ya viambishi vya nafsi na njeo katika vitenzi vya lugha ya Kifipa. Baada ya utangulizi na maelezo kuhusu nadharia iliyotumika, sehemu inayofuata ni uwasilishaji wa data kama zilivyopatikana uwandani na kuchanganuliwa na watafiti.

**Viambishi vya Nafsi katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa**

Massamba (2004) anaeleza viambishi vya nafsi kuwa ni mofimu funge ambazo hupachikwa katika kitenzi kuwakilisha nafsi katika tungo. Kapinga (1983) na Massamba (2004) walibainisha kuwa, katika lugha ya Kiswahili kuna nafsi tatu ambazo ni nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu (nafsi ya I, II, na III) zenye umoja na wingi. Katika nafsi ya kwanza umoja, mzungumzaji anajirejelea

yeye mwenyewe ilhali katika nafsi ya kwanza wingi, mzungumzaji anarejelea kundi la watu ambalo yeye ni sehemu yake. Kwa upande wa nafsi ya pili umoja, mzungumzaji anamrejelea mtu ambaye yupo karibu naye kiasi kwamba anamuona kwa macho, vivyo hivyo kwa nafsi ya pili wingi ambapo mzungumzaji anawarejelea kundi la watu ambalo yupo karibu nalo lakini yeye siyo sehemu ya kundi hilo kama ilivyo kwa nafsi ya kwanza wingi. Aidha, nafsi ya tatu umoja na wingi, mzungumzaji anamrejelea mtu au kundi la watu ambalo lipo mbali naye kiasi kwamba hawezi kuliona (taz. Massamba, 2004; Matinde, 2012).

Massamba (2004) na Matinde (2012) wanaendelea kueleza kuwa nafsi hizo hufanya kuwapo kwa maneno sita yanayoziwakilisha ambayo ni mimi na sisi (nafsi ya kwanza umoja na wingi), wewe na nyinyi (nafsi ya pili umoja na wingi) na yeye na wao (nafsi ya tatu umoja na wingi). Katika vitenzi vya Kiswahili, nafsi hizo husetiriwa na viambishi {ni-}, {tu-}, {u-}, {m-}, {a-} na {wa-} mtawalia (taz. Kapinga, 1983; Wesana-Chomi, 2003; Massamba, 2004; Mgullu, 2010; Matinde, 2012). Kwa upande wa lugha ya Kifipa, kuna nafsi tatu zenye umoja na wingi; nafsi ya kwanza umoja na wingi, nafsi ya pili umoja na wingi na nafsi ya tatu umoja na wingi. Nafsi hizo zina maneno yanayoziwakilisha ambayo ni *nene* (mimi), *sweswe* (sisi), *wewe* (wewe), *mwemwe* (nyingi), *wiwi* (yeye) na *ayakola* (wao). Nafsi hizo husetiriwa na viambishi mbalimbali kwenye vitenzi kama itakavyojidhihirisha kwenye uchambuzi wa nafsi moja baada ya nyingine kwenye sehemu zinazofuata.

**Nafsi ya Kwanza Umoja (NfsIu) katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa**

Katika lugha ya Kifipa neno *nene* (mimi) ndilo kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja. Kwenye vitenzi vya lugha tajwa, neno hilo husetiriwa na viambishi viwili tofauti. Viambishi hivyo ni **{Na-}** na **{N-}.** Tazama mifano ifuatayo:

| **Lugha ya Kifipa** | **Tafsiri ya Kiswahili** |
|---|---|
| 1. **Na** - a - sek - ile<br>NfsIu Njwl Mzz Njwl | Nilicheka |
| 2. **N** - du - sak - a<br>NfsIu Njwp Mzz Ii | Ninaoa |
| 3. **N** - du - lim - a<br>NfsIu Njwj Mzz Ii | Nitalima |

**Chanzo**: Data za uwandani (2022)

Kutokana na data namba 1 - 3 hapo juu, viambishi vilivyokozwa wino ambavyo ni **{Na-}** katika kitenzi *Naasekile* (Nilicheka) na **{N-}** katika vitenzi *Ndusaka* (Ninaoa) na *Ndulima* (Nitalima) vinasetiri nafsi ya kwanza umoja katika vitenzi vya lugha ya Kifipa. Ubainishaji wa viambishi hivyo umeongozwa na msingi wa NABA ulioteuliwa. Kutokana na uchanganuzi wa data za utafiti huu, imebainika kuwa kiambishi cha nafsi ambacho kinatokana na mchakato wa uambishaji kinatokea mbali na mzizi wa kitenzi. Vilevile, kiambishi hiki hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi.

**Nafsi ya kwanza wingi (NfsIw) katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa**

Kiwakilishi cha nafsi hii katika lugha iliyotafitiwa ni *sweswe* (sisi) na kuna kiambishi kimoja kinachosetiri nafsi hiyo kwenye vitenzi. Kiambishi hicho ni **{Tu-}**. Mifano ifuatayo inaonesha kiambishi cha nafsi ya kwanza wingi katika vitenzi vya lugha ya Kifipa.

| **Lugha ya Kifipa** | **Tafsiri ya Kiswahili** |
|---|---|
| 4. **Tw** - a - lund - ile<br>NfsIw Njwl Mzz Njwl | Tuliimba |
| 5. **Tu** - lu - lim - a<br>NfsIw Njwp Mzz Ii | Tunalima |
| 6. **Tu** - lu - sak - a<br>NfsIw Njwj Mzz Ii | Tutaoa |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Data namba 4 - 6 hapo juu zinaonesha viambishi vya nafsi ya kwanza wingi katika vitenzi vya lugha ya Kifipa. Viambishi hivyo vimejitokeza viwili japo ni nafsi ileile (nafsi ya kwanza wingi). Viambishi hivyo ni **{Tw-}** katika kitenzi *Twalundile* (Tuliimba) na **{Tu-}** katika vitenzi *Tululima* (Tunalima) na *Tulusaka* (Tutaoa). Kimsingi kiambishi **{Tw-}** siyo kiambishi tofauti bali ni kiambishi kilekile **{Tu-}** tulichobainisha tangu awali kuwa ndicho husetiri nafsi ya pili wingi. Kilichotokea hapo ni michakato ya kifonolojia ambapo fonimu /**u**/ hubadilika na kuwa kiyeyusho /**w**/ katika mazingira ya kufuatiwa na fonimu /**a**/. Kwa hiyo badala ya kitenzi kutamkwa *Tualundile* kinatamkwa *Twalundile*.

**Nafsi ya Pili Umoja (NfsIIu) katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa**

Neno linalowakilisha nafsi hii katika lugha iliyotafitiwa ni *wewe* (wewe). Nafsi hii katika vitenzi vya lugha ya Kifipa husetiriwa na kiambishi kimoja kama ilivyo kwa nafsi ya kwanza wingi iliyochambuliwa hapo juu. Kiambishi kinachowakilisha nafsi ya pili umoja kwenye lugha ya Kifipa ni **{U-}.** Tazama mifano ifuatayo:

| Lugha ya Kifipa | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|
| 7. **W** - a - sek - ile<br>NfsIIu Njwl Mzz Njwl | Ulicheka |
| 8. **U** - lu - lund - a<br>NfsIIu Njwp Mzz Ii | Unaimba |
| 9. **U** - lu - sak - a<br>NfsIIu Njwj Mzz Ii | Utaoa |

**Chanza:** Data za Uwandani (2022)

Katika data hapo juu, viambishi vilivyokozwa wino ndivyo viambishi vya nafsi ya pili umoja. Viambishi hivyo ni **{W-}** katika kitenzi *Wasekile* (Ulicheka) na **{U-}** katika vitenzi *Ululunda* (Unaimba) na *Ulusaka* (Utaoa). Kama tulivyoeleza wakati wa kubainisha kiambishi cha nafsi ya kwanza wingi, vilevile katika data namba 7 - 9 hapo juu viambishi vya nafsi ya pili umoja vinaonekana kuwa viwili yaani **{W-}** na **{U-}**. Kimsingi kilichopo hapo siyo viambishi viwili tofauti bali ni kiambishi kilekile tulichobainisha kuwa kinawakilisha nafsi ya pili wingi ambacho ni **{U-}**. Mazingira ya utokeaji wa kiambishi **{W-}** kwenye kitenzi *Wasekile* yanafanana na mazingira ya utokeaji wa kiambishi **{Tw-}** kwenye kitenzi *Twalundile* kama tulivyoeleza hapo juu ambapo ni mchakato wa uyeyushaji uliohusika katika viambishi hivyo. Hii ina maana kwamba fonimu /**u**/ hubadilika na kuwa kiyeyusho /**w**/ katika mazingira ya kufuatiwa na fonimu /**a**/. Hivyo basi, kitenzi badala ya kutamkwa *Uasekile* kinatamkwa *Wasekile* ili kurahisisha matamshi kifonolojia.

**Nafsi ya Pili Wingi (NfsIIw) katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa**

Wakati wa uchanganuzi wa data za vitenzi vya lugha ya Kifipa vilivyokusanywa uwandani, imebainika kuwa neno linalowakilisha nafsi ya pili wingi ni *mwemwe* (nyinyi). Na kiambishi kinachowakilisha nafsi hiyo katika vitenzi vya lugha husika ni **{Mu-}** kama ambavyo kinabainika kupitia mifano hapa chini.

| Lugha ya Kifipa | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|
| 10. **Mw** - a - lim - ile<br>NfsIIw Njwl Mzz Njwl | Mlilima |
| 11. **Mu** - lu - sak - a<br>NfsIIw Njwp Mzz Ii | Mnaoa |
| 12. **Mu** - lu - lund - a<br>NfsIIw Njwj Mzz Ii | Mtaimba |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Mifano katika namba 10 - 12 hapo juu imebainisha viambishi vya nafsi ya pili wingi katika vitenzi vya lugha ya Kifipa. Viambishi hivyo vimekozwa wino ili kurahisisha kuvibainisha. Viambishi hivyo

ni **{Mw-}** katika kitenzi *mwalimile* (mlilima), na **{Mu-}** katika vitenzi *mulusaka* (mnaoa) na *mululunda* (mtaimba). Kama tulivyoeleza wakati wa kubainisha viambishi vya nafsi ya kwanza wingi na nafsi ya pili umoja, vilevile mchakato wa kifonolojia wa uyeyushaji umehusika kuvifanya viambishi vya nafsi ya pili wingi vionekane kuwa viwili ilhali kiambishi **{Mw-}** ni kilekile kilichobainishwa kuwa ndicho husetiri nafsi ya pili wingi ambacho ni **{Mu-}.**

**Nafsi ya Tatu Umoja (NfsIIIu) katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa**

Nafsi hii katika lugha ya Kifipa huwakilishwa na neno *wiwi* (yeye). Nafsi hiyo katika vitenzi vya lugha iliyotafitiwa (Kifipa) huwakilishwa na viambishi viwili tofauti kwenye vitenzi ambavyo ni **{Wa}** na **{A-}.** Mifano ifuatayo inabainisha viambishi hivyo katika vitenzi.

| **Lugha ya Kifipa** | **Tafsiri ya Kiswahili** |
|---|---|
| 13. **Wa** - a - sak - ile<br>NfsIIIu Njwl Mzz Njwl | Alioa |
| 14. **A** - lu - lund - a<br>NfsIIIu Njwp Mzz Ii | Anaimba |
| 15. **A** - lu - lim - a<br>NfsIIIu Njwj Mzz Ii | Atalima |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Kama data inavyoonekana hapo juu, vilivyokozwa wino ndivyo viambishi vya nafsi ya tatu umoja kwenye vitenzi vya lugha ya Kifipa. Viambishi hivyo ni **{Wa-}** katika kitenzi *waasakile* (alioa) na **{A-}** katika vitenzi *alulunda* (anaimba) na *alulima* (atalima). Katika viambishi viwili vinavyowakilisha nafsi ya tatu umoja (**{Wa-}** na **{A-}**), kiambishi **{Wa-}** hutokea katika vitenzi vya njeo ya wakati uliopita. Kwa upande mwingine kiambishi **{A-}** hutokea katika vitenzi vyenye njeo ya wakati uliopo na ujao.

**Nafsi ya Tatu Wingi (NfsIIIw) katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa**

Kutokana na data za utafiti huu imebainika kuwa nafsi ya tatu umoja inawakilishwa na neno *ayakola* (wao) ambapo kiambishi chake kwenye vitenzi ni **{Ya-}.** Tazama mifano ifuatayo kwa udhihirisho zaidi.

| **Lugha ya Kifipa** | **Tafsiri ya Kiswahili** |
|---|---|
| 16. **Ya** - a - lim - ile<br>NfsIIIw Njwl Mzz Njwl | Walilima |
| 17. **Ya** - lu - lund - a<br>NfsIIIw Njwp Mzz Ii | Wanaimba |
| 18. **Ya** - lu - sek - a<br>NfsIIIw Njwj Mzz Ii | Watacheka |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Kutokana na data hapo juu, kiambishi kilichokozwa wino **{Ya-}** katika maneno *yaalimile* (walilima), *yalulunda* (wanaimba) na *yaluseka* (watacheka) ndicho kiambishi kinachowakilisha nafsi ya tatu wingi katika vitenzi vya lugha ya Kifipa. Kiambishi hicho hutokea mbali na mzizi wa kitenzi kutokana na mchakato wa uambishaji kama madai ya msingi wa NABA uliotumika katika uchanganuzi wa data za utafiti huu yalivyo. Nafsi ya tatu wingi katika lugha ya Kifipa ndiyo nafsi pekee yenye kiambishi kimoja kinachodhihirika kwa umbo moja kwa njeo zote kwani nafsi zingine zina viambishi viwiliviwili tofauti kwa nafsi moja (nafsi ya kwanza umoja na nafsi ya tatu umoja). Kwa upande mwingine nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili umoja na wingi zina kiambishi kimoja cha nafsi kinachodhihirika katika maumbo mawili tofauti kutokana na michakato ya kifonolojia yaani uyeyushaji kulingana na njeo za vitenzi husika.

**Viambishi vya Njeo katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa**

Massamba (2004) anaeleza njeo kuwa ni kipengele cha kisarufi kinachoonesha uhusiano kati ya nafsi mbili za wakati. Anaendelea kueleza kuwa tukichukulia mfano wa matukio mawili, moja likiwa limetokea katika wakati $\mathbf{W_1}$ na jingine likatokea wakati $\mathbf{W_2}$, njeo ndiyo ituambiayo kama $\mathbf{W_1}$ ulikuwa kabla ya wakati $\mathbf{W_2}$, viliingiliana au ulikuja baada ya $\mathbf{W_1}$. Anafafanua zaidi kuwa kimapokeo mara nyingi dhana hii hugawanywa katika nyakati kuu tatu: wakati uliopo, uliopita na ujao. Kimsingi kinachoelezwa na mtaalamu huyu ni kuhusu namna ya kulizungumzia tukio lililofanyika, linalofanyika au litakalofanyika ambapo dhana hiyo kiisimu ndiyo hujulikana kama njeo.

Kuhusu viambishi vya njeo, Massamba (2004) anaeleza kuwa ni mofimu funge, katika kitenzi, ambazo huonesha ni lini tendo fulani lilifanyika, linafanyika au litafanyika. Kuna viambishi mahususi vinavyowakilisha kila njeo kwenye vitenzi vya lugha ya Kiswahili. Wesana-Chomi (2003; 2013); Mgullu (2010); Matinde (2012); na TET (2019) wamebainisha viambishi vitatu vinavyosetiri njeo katika vitenzi vya lugha ya Kiswahili. Viambishi hivyo ni **{-li-}** (wakati uliopita), **{-na-}** (wakati uliopo) na **{-ta-}** (wakati ujao). Viambishi vya njeo vilivyobainishwa na wataalamu hao ni vya kitenzi yakinishi na si vya hali nyingine za kitenzi kama vile hali ya mazoea, hali ya ukanushi, hali timilifu na hali ya masharti.

Matokeo ya utafiti huu kwa upande mwingine yameonesha kuwa, lugha ya Kifipa kwa vitenzi yakinishi ina nyakati kuu tatu. Nyakati hizo ni wakati uliopita, wakati uliopo na wakati ujao. Wakati uliopita na wakati uliopo zina viambishi mahususi vinavyozisetiri kwenye vitenzi vya lugha iliyotafitiwa. Mathalani, viambishi vinavyosetiri wakati uliopita ni **{-a-}** na **{-ile}** ambavyo hutokea kwa pamoja kwenye kitenzi na kiambishi kinachosetiri wakati uliopo ni **{-lu-}**. Wakati ujao katika lugha ya Kifipa hauna kiambishi maalumu bali masuala ya kifonolojia (toni[2]) ndiyo hutumika kubainisha wakati huo kwa kutumia kitenzi cha wakati uliopo. Nyakati hizo zinachambuliwa mmoja baada ya mwingine kwenye sehemu inayofuata.

**Njeo ya Wakati Uliopita (Njwl) katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa**

Kama ilivyo kwenye lugha mbalimbali kuwa wakati uliopita hudokeza tukio au matukio yaliotokea kipindi kilichopita, vilevile kwa mujibu wa data za utafiti huu, katika lugha ya Kifipa wakati uliopita humaanisha tukio au matukio yaliyopita. Inaweza kuwa kuanzia jana, juzi, wiki iliyopita au miezi na miaka iliyopita. Kama tulivyodokeza hapo juu, njeo hii husetiriwa na viambishi **{-a-}** na **{-ile}** katika vitenzi vya lugha ya Kifipa. Tazama mifano ifuatayo kwa udhihirisho zaidi kwa nafsi zote sita (Nafsi ya kwanza umoja, ya kwanza wingi, ya pili umoja, ya pili wingi, ya tatu umoja na ya tatu wingi).

| **Lugha ya Kifipa** | **Tafsiri ya Kiswahili** |
|---|---|
| 19. Na - **a** - sek - **ile**<br>NfsIu Njwl Mzz Njwl | Nilicheka |
| 20. Tw - **a** - lund - **ile**<br>NfsIw Njwl Mzz Njwl | Tuliimba |
| 21. W - **a** - sak - **ile**<br>NfsIIu Njwl Mzz Njwl | Ulioa |
| 22. Mw - **a** - lim - **ile**<br>NfsIIw Njwl Mzz Njwl | Mlilima |
| 23. Wa - **a** - sek - **ile**<br>NfsIIIu Njwl Mzz Njwl | Alicheka |

[2] Toni ni sifa inayowakilisha kiwango pambanuzi cha kidatu cha silabi katika neno au sentensi na ambayo huweza kubadili maana ya neno au sentensi hiyo kisemantiki au kisarufi (Massamba, 2004; Mgullu, 2010). Alama ya toni ni ′ kwa tonipanda na ` kwa tonishuka.

24. Ya - **a** - lund - **ile** Waliimba
NfsIIIw Njwl Mzz Njwl

**Chanzo**: Data za Uwandani (2022)

Kutokana na data hapo juu, viambishi **{-a-}** na **{-ile}** vilivyokozwa wino ndivyo husetiri njeo ya wakati uliopita kwenye vitenzi vya lugha ya Kifipa. Ubainishaji wa viambishi hivyo umeongozwa na msingi wa NABA. Kwa mujibu wa data za utafiti huu, viambishi vya njeo ya wakati uliopita vimetokana na mchakato wa uambishaji ambao huongeza sifa za kisarufi kwenye kitenzi bila kubadili maana ya msingi ya kitenzi kilichoambishwa. Viambishi hivyo vimetokea karibu na mzizi wa kitenzi. Kiambishi **{-a-}** kinatokea kabla ya mzizi wa kitenzi ilhali kiambishi **{-ile}** kinatokea baada ya mzizi wa kitenzi.

Katika lugha ya Kifipa njeo ya wakati uliopita husetiriwa na viambishi viwili tofauti vinavyotokea kwa pamoja kwenye kitenzi kimoja. Suala hili siyo geni katika lugha za Kibantu kwani utafiti wa Lusekelo (2007:67) katika lugha ya Kinyakyusa ulionesha matokeo ya namna hiyo ambapo kiambishi **{-a-}** hutokea kwa pamoja na kiambishi **{-ile}** kuwakilisha njeo ya wakati uliopita kwa mfano; *Bha-**a**-tiim-**ile*** (Walichunga). Vilevile utafiti wa Ngenzi (2016:61) katika lugha ya Kihehe ulionesha kuwa kiambishi **{-ka-}** hutokea kwa pamoja na kiambishi **{-ile}** kuwakilisha njeo ya wakati uliopita kwa mfano; Tu-**ka**-yav-**ile** (Tulichimba).

**Njeo ya Wakati Uliopo (Njwp) katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa**

Njeo hii katika lugha ya Kifipa hurejelea tukio au matukio yanayoendelea kufanyika muda huohuo. Hii ina maana kwamba mtu au watu wanaorejelewa kufanya shughuli hiyo wanaendelea kuifanya wakati huo. Katika lugha hii, njeo ya wakati uliopo huwakilishwa na kiambishi **{-lu-}** huku irabu ishilizi ya maana ikiwa ya tonishuka **{-à}**. Ifuatayo ni mifano ya udhihirisho wa kiambishi cha njeo husika katika vitenzi vya lugha ya Kifipa.

**Lugha ya Kifipa** **Tafsiri ya Kiswahili**

25. N - **du** - lim - à Ninalima
NfsIu Njwp Mzz Ii

26. Tu - **lu** - sak - à Tunaoa
NfsIw Njwp Mzz Ii

27. U - **lu** - lund - à Unaimba
NfsIIu Njwp Mzz Ii

28. Mu - **lu** - sek - à Mnacheka
NfsIIw Njwp Mzz Ii

29. A - **lu** - sak - à Anaoa
NfsIIIu Njwp Mzz Ii

30. Ya - **lu** - lim - à Wanalima
NfsIIIw Njwp Mzz Ii

**Chanzo**: Data za Uwandani (2022)

Data hapo juu zinaonesha kiambishi kinachowakilisha njeo ya wakati uliopo katika vitenzi vya lugha ya Kifipa. Kiambishi hicho ni **{-lu-}** huku irabu ishilizi ikiwa ya tonishuka **{-à}**. Katika uchanganuzi wa data imebainika kuwa **{-lu-}** ndicho kiambishi cha njeo ya wakati uliopo katika vitenzi vya lugha tajwa. Njeo hiyo hiyo katika nafsi ya kwanza umoja imesetiriwa na kiambishi **{-du-}** tofauti na nafsi nyingine tano zilizosalia ambazo zote zimesetiriwa na kiambishi **{-lu-}**. Kimsingi kilichofanyika hapo siyo kwamba ni kiambishi tofauti, bali ni masuala ya kifonolojia. Hii ina maana kwamba fonimu **/l/** hubadilika na kuwa **/d/** katika mazingira ya kutanguliwa na nazali **/n/**. Mgullu (2010) na Matinde (2012) wameuita mchakato huu kuwa ni kuimarika kwa fonimu ambapo fonimu inayotumia nguvu kidogo wakati wa utamkaji huanza kutumia nguvu zaidi. Katika mchakato huu kitambaza **/l/** kinachotumia nguvu kidogo wakati wa utamkaji kimebadilika na kuwa kizuiwa ghuna **/d/** kinachotumia nguvu zaidi wakati wa utamkaji ambalo ni tendo la kuimalika kwa fonimu. Kwa

hiyo tunaweza kusema kuwa kiambishi **{-lu-}** kinaweza kujitokeza pia katika umbo la nje kama kiambishi **{-du-}** kutokana na michakato ya kifonolojia.

**Njeo ya Wakati Ujao (Njwj) katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa**

Katika vitenzi vya lugha ya Kifipa, wakati ujao hudokeza tendo litakalofanywa kipindi kijacho. Kipindi hicho kinaweza kuwa kesho na kuendelea. Katika lugha ya Kifipa ubayana wa kipindi hicho huweza kutambuliwa kwa maneno (vielezi vya wakati) yanayoambatana na kipindi kinachodokezwa. Mfano; *Ma:lume alulimá echalo iyulu* (Mjomba atalima shamba kesho) au *Ma:lume alulimá echalo mwaka unje* (Mjomba atalima shamba baada ya miaka mingi sana ijayo. Kama tulivyodokeza hapo awali, njeo hii haina kiambishi maalumu kinachoisetiri. Kwa hiyo, hutumia kiambishi cha njeo ya wakati uliopo ambapo masuala ya kifonolojia (toni) huhusika kuweka ubayana wa njeo inayozungumzwa. Tazama mifano ifuatayo:


| Lugha ya Kifipa | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|
| 31. N - **du** - lim - á<br>NfsIu Njwj Mzz Ii | Nitalima |
| 32. Tu - **lu** - sak - á<br>NfsIw Njwj Mzz Ii | Tutaoa |
| 33. U - **lu** - lund - á<br>NfsIIu Njwj Mzz Ii | Utaimba |
| 34. Mu - **lu** - sek - á<br>NfsIIw Njwj Mzz Ii | Mtacheka |
| 35. A - **lu** - lim - á<br>NfsIIIu Njwj Mzz Ii | Atalima |
| 36. Ya - **lu** - sak - á<br>NfsIIw Njwj Mzz Ii | Wataoa |

**Chanzo**: Data za Uwandani (2022)

Kutokana na mifano hapo juu, kiambishi **{-lu-}** kilichokolezwa wino ambacho ni kiambishi cha njeo ya wakati uliopo, ndicho kiambishi kinachowakilisha njeo ya wakati ujao katika vitenzi vya lugha ya Kifipa. Kama ilivyodokezwa hapo juu, njeo hii haina kiambishi mahususi kinachoiwakilisha kwenye vitenzi bali hutumia masuala ya kifonolojia (toni) ili kukibainisha. Katika utamkaji wa kitenzi ambacho kipo katika muundo wa njeo ya wakati uliopo irabu ishilizi ya maana hupachikwa tonipanda kumaanisha tendo litafanyika wakati ujao.

Kifuatacho ni kielelezo kuonesha njeo za lugha ya kifipa na viambishi vinavyoziwakilisha njeo hizo kwenye vitenzi.

**Kielelezo na 1: Njeo za lugha ya Kifipa na viambishi vinavyoziwakilisha kwenye vitenzi**




**Chanzo**: Data za Uwandani (2022)

Kielelezo hapo juu kinaonesha njeo za lugha ya Kifipa na viambishi vinavyoziwakilisha. Kielelezo hicho kimetokana na uchanganuzi wa data za utafiti huu zilizopatikana uwandani.

**Ruwaza ya Viambishi vya Nafsi na Njeo katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa**

Kutokana na data za utafiti huu zilizochanganuliwa kwa msingi wa NABA unaodai kuwa utokeaji wa viambishi na mfuatano wake unatawaliwa na kanuni maalumu za kimofolojia za sarufi ya lugha husika, imebainika kuwa viambishi vya nafsi na njeo katika vitenzi vya lugha ya Kifipa havijitokezi kiholela, bali kuna taratibu maalumu za kimofolojia zinazoamua kiambishi kipi kitokee wapi na kipi kitangulie kutokea na kipi kifuate. Ili kurahisisha ufafanuzi wa ruwaza za viambishi lengwa katika lugha iliyotafitiwa, tumeamua kufafanua ruwaza hizo katika makundi makuu matatu; viambishi vyote vya nafsi (nafsi ya kwanza umoja, nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili umoja, nafsi ya pili wingi, nafsi ya tatu umoja na nafsi ya tatu wingi) na njeo ya wakati uliopita, viambishi vyote vya nafsi na njeo ya wakati uliopo na viambishi vyote vya nafsi na njeo ya wakati ujao. Sehemu inayofuata inatoa ufafanuzi huo kwa kundi moja baada ya jingine.

**Ruwaza ya Viambishi vya Nafsi na Njeo ya Wakati Uliopita katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa**

Katika lugha ya Kifipa kiambishi cha nafsi hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi ilhali viambishi vya njeo ya wakati uliopita hutokea kabla na baada ya mzizi wa kitenzi. Viambishi vya njeo ya wakati uliopita hutokea karibu na mzizi wa kitenzi (kiambishi **{-a-}** kabla ya mzizi na kiambishi **{-ile}** baada ya mzizi) ilhali viambishi vya nafsi hutokea mbali na mzizi wa kitenzi kama madai ya msingi wa NABA yalivyo kwamba, katika mchakato wa uambishaji kuna viambishi hutokea karibu na mzizi wa kitenzi na vingine hutokea mbali kutokana na uhusiano wa kimaana na sarufi ya lugha husika. Tazama ruwaza ya viambishi hivyo kwa baadhi ya vitenzi kwenye mfano ufuatao:

| **Lugha ya Kifipa** | **Tafsiri ya Kiswahili** |
|---|---|
| 37. **Na** - *a* - sak - *ile*<br>NfsIu Njwl Mzz Njwl | Nilioa |
| 38. **W** - *a* - lund - *ile*<br>NfsIIu Njwl Mzz Njwl | Uliimba |
| 39. **Ya** - *a* - lim - *ile*<br>NfsIIIw Njwl Mzz Njwl | Walilima |

**Chanzo:** Data za Uwandani (2022)

Katika data hapo juu, viambishi vilivyokozwa wino ambavyo ni **{Na-}** katika kitenzi *Naasakile* (Nilioa), **{W-}** katika kitenzi *Walundile* (Uliimba) na **{Ya-}** katika kitenzi *Yaalimile* (Walilima) vinawakilisha nafsi na vile vilivyoandikwa kwa hati mlazo ambavyo ni *{-a-}* na *{-ile}* kwenye vitenzi vyote hapo juu vinawakilisha njeo ya wakati uliopita katika vitenzi vya lugha ya Kifipa. Madai ya msingi wa NABA yameweza kudhihirika katika matokeo ya utafiti huu kuwa utokeaji wa viambishi katika lugha si wa kiholela bali hufuata kanuni maalumu za sarufi ya lugha husika. Kifuatacho ni kielelezo cha ruwaza ya viambishi vya nafsi na njeo katika vitenzi vya lugha ya Kifipa katika njeo ya wakati uliopita.

**Kielelezo na. 2: Ruwaza ya Viambishi vya Nafsi na Njeo katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa kwa Njeo ya Wakati uliopita**

| |
|---|
| NFS + NJWL+MZZ + NJWL |

Kielelezo namba mbili (2) hapo juu kinaonesha ruwaza ya viambishi vya nafsi na njeo katika vitenzi vya lugha ya Kifipa. Kielelezo hicho kinaakisi maelezo yaliyotolewa hapo juu kuhusu ruwaza ya viambishi husika kwenye njeo ya wakati uliopita.

**Ruwaza ya Viambishi vya Nafsi na Njeo ya Wakati Uliopo katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa**
Kwa kuongozwa na msingi wa NABA, tumebaini kuwa katika lugha ya Kifipa viambishi vya nafsi na njeo ya wakati uliopo vyote hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi. Katika ruwaza hiyo kiambishi cha nafsi hutokea katika nafasi ya kwanza na kufuatiwa na kiambishi cha njeo ya wakati uliopo na baada ya hapo mzizi hutokea. Hii ina maana kwamba katika njeo ya wakati uliopo kiambishi cha njeo hutokea karibu zaidi na mzizi wa kitenzi kuliko kiambishi cha nafsi. Mifano ifuatayo inadhihirisha ruwaza ya viambishi hivyo katika lugha iliyotafitiwa.

| **Lugha ya Kifipa** | **Tafsiri ya Kiswahili** |
|---|---|
| 40. **Tu** - *lu* - lund - à<br>NfsIw Njwp Mzz Ii | Tunaimba |
| 41. **U** - *lu* - sek - à<br>NfsIIu Njwp Mzz Ii | Unacheka |
| 42. **A** - *lu* - sak - à<br>NfsIIIu Njwp Mzz Ii | Anaoa |

**Chanzo**: Data za Uwandani (2022)

Kutokana na data namba 40, 41 na 42 hapo juu, viambishi vilivyokozwa wino ambavyo ni **{Tu-}** katika neno *Tululunda* (Tunaimba), **{U-}** katika neno *Uluseka* (Unacheka) na **{A-}** katika neno *Alusaka* (Anaoa) vinawakilisha viambishi vya nafsi katika njeo ya wakati uliopo. Kwa upande mwingine viambishi vilivyoandikwa kwa hati mlazo vinawakilisha kiambishi cha njeo ya wakati uliopo ambacho ni *{-lu-}* huku irabu ishirizi ya maana ikiwa ya tonishuka. Tofauti na ruwaza ya viambishi vya nafsi na njeo ya wakati uliopita katika lugha ya Kifipa ambapo kiambishi cha nafsi na kiambishi kimojawapo cha njeo hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi na kiambishi kingine cha njeo ya wakati uliopita hutokea baada ya mzizi wa kitenzi, katika njeo ya wakati uliopo, viambishi vyote hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi. Kielelezo kifuatacho kinaonesha ruwaza ya viambishi vya nafsi na njeo katika vitenzi vya lugha ya Kifipa kwa njeo ya wakati uliopo.

**Kielelezo na. 3:** **Ruwaza ya Viambishi vya Nafsi na Njeo katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa kwa Njeo ya Wakati uliopo**

| |
|---|
| NFS + NJ +MZZ + Ii |

Kielelezo namba tatu (3) hapo juu kinaonesha ruwaza ya viambishi vya nafsi na njeo ya wakati uliopo katika vitenzi vya lugha ya Kifipa. Kielelezo hicho kinaakisi maelezo yaliyotolewa hapo juu kuhusu ruwaza ya viambishi husika kwenye njeo ya wakati uliopo.

**Ruwaza ya Viambishi vya Nafsi na Njeo ya Wakati Ujao katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa**
Kama tulivyobainisha tangu awali, viambishi vya nafsi na njeo vinavyotumika katika njeo ya wakati uliopo ndivyo hivyohivyo vinavyotumika katika njeo ya wakati ujao katika lugha ya Kifipa. Utofauti uliopo ni katika mambo ya kifonolojia (toni). Katika lugha ya Kifipa viambishi vyote (vya nafsi na njeo ya wakati ujao) hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi. Kiambishi cha nafsi kinatokea katika nafasi ya kwanza kikifuatiwa na kiambishi cha njeo ya wakati ujao. Kiambishi cha njeo ya wakati ujao hutokea karibu zaidi na mzizi wa kitenzi kuliko kiambishi cha nafsi. Pamoja na msingi wa NABA uliotumika kueleza ruwaza ya viambishi husika, masuala ya kifonolojia yalikuwa muhimu sana ukizingatia kwamba viambishi vyote vinavyotumika kubainisha nafsi na njeo ya wakati uliopo ndivyo vinavyotumika kubainisha nafsi na njeo ya wakati ujao. Tazama mifano ifuatayo kwa udhihirisho zaidi wa ruwaza iliyofafanuliwa:

| **Lugha ya Kifipa** | **Tafsiri ya Kiswahili** |
|---|---|
| 43. **N** - *du* - lim - á<br>NfsIu Njwj Mzz Ii | Nitalima |
| 44. **Mu** - *lu* - sak - á<br>NfsIIw Njwj Mzz Ii | Mtaoa |
| 45. **Ya** - *lu* - sek - á<br>NfsIIIw Njwl Mzz Ii | Watacheka |

**Chanzo**: Data za Uwandani (2022)

Kwa mujibu wa data 43, 44 na 45 hapo juu, viambishi vilivyokozwa wino ambavyo ni **{N-}** cha nafsi ya kwanza umoja katika neno *Ndulima* (Nitalima), **{Mu-}** cha nafsi ya pili wingi katika neno *Mulusaka* (Mtaoa) na **{Ya-}** cha nafsi ya tatu wingi katika neno *Yaluseka* (Watacheka) vinawakilisha viambishi vya nafsi katika njeo ya wakati ujao. Kwa upande mwingine viambishi vilivyoandikwa kwa hati mlazo vinawakilisha kiambishi cha njeo ya wakati ujao ambacho ni *{-lu-}* kinachoenda sambamba na irabu ishilizi ya maana yenye tonipanda **{-á}**. Kimsingi utamkaji wa tonipanda wa irabu ishilizi ya maana ndiyo unaoleta tofauti ya kitenzi cha wakati uliopo na ujao. Ruwaza ya viambishi vya nafsi na njeo ya wakati ujao kimofolojia katika lugha ya Kifipa ndiyo ileile ya wakati uliopo kwani kiambishi cha nafsi na kiambishi cha njeo hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi. Kielelezo kifuatacho kinaonesha ruwaza ya viambishi vya nafsi na njeo katika vitenzi vya lugha ya Kifipa kwa njeo ya wakati ujao.

**Kielelezo na. 4: Ruwaza ya Viambishi vya Nafsi na Njeo katika Vitenzi vya Lugha ya Kifipa kwa Njeo ya Wakati Ujao**

NFS + NJ +MZZ + Ii

Kielelezo namba nne (4) hapo juu kinaonesha ruwaza ya viambishi vya nafsi na njeo katika vitenzi vya lugha ya Kifipa. Kielelezo hicho kinatokana na maelezo yaliyotolewa hapo juu kuhusu ruwaza ya viambishi husika kwenye njeo ya wakati ujao. Ukiangalia kielelezo namba tatu na namba nne vinafanana. Hii inatokana na ruwaza ya njeo hizo kufanana kimofolojia na kutofautishwa kifonolojia kama tulivyoeleza hapo juu wakati wa ubainishaji wa viambishi vya njeo ya wakati uliopo.

### Hitimisho

Makala haya ni matokeo ya utafiti uliofanyika kuchunguza ruwaza ya viambishi vya nafsi na njeo katika lugha ya Kifipa. Baada ya kuchanganua data imebainika kuwa, lugha ya Kifipa ina nafsi tatu zenye umoja na wingi. Nafsi ya kwanza umoja na nafsi ya tatu umoja huwakilishwa na viambishi viwiliviwili ambavyo ni **{Na-}** na **{N-}** kwa nafsi ya kwanza umoja na **{Wa-}** na **{A-}** kwa nafsi ya tatu umoja. Nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili umoja na wingi na nafsi ya tatu wingi huwakilishwa na kiambishi kimojakimoja. Viambishi hivyo ni **{Tu-}, {U-}, {Mu-}** na **{Ya-}** mtawalia. Viambishi vyote vya nafsi hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi. Kwa upande wa njeo, lugha ya Kifipa ina njeo tatu; wakati uliopita, uliopo na ujao. Wakati uliopita na uliopo zina viambishi bayana ilhali wakati ujao huamriwa na masuala ya kifonolojia kwa kutumia umbo la kitenzi cha wakati uliopo. Wakati uliopita una viambishi viwili ambavyo ni **{-a-}** na **{-ile}** vinavyotokea kwa pamoja kwenye kitenzi ambapo kiambishi kimoja **{-a-}** hutokea kabla ya mzizi na kingine **{-ile}** hutokea baada ya mzizi. Kiambishi cha wakati uliopo **{-lu-}** hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi.

**Marejeleo**


Baker, M. C. (1985). "The Mirror Principle and Morphosyntactic Explanation". Katika *Lingustics Enquiry,* Juz.16: 373- 414.

Baker, M. C. (1988). *Incorparation: a theory of grammatical function changing.* Chicago: Chicago University Press.

Baker, M. C. (2002). "Building and Merging, not Checking: The Nonexistence of (AUX)-S-V-O Languages". Katika *Lingustics Enquiry,* Juz.33: 321-328.

Batibo, H.M. (2010). "Uchunguzi katika Sarufi ya Kiswahili na Lugha zinazohusiana". Katika TUKI (Mh.) *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili I*. Dar es Salaam: TUKI. Kur.188-218.

Charwi, M.Z. (2010). "Viambishi Nafsi katika Muundo wa Kitenzi cha Kikuria". *Utafiti*, Juz. 14 (2): 339 – 352.

Habwe, J na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Kapinga, M.C. (1983) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B. na Msanjila, Y.P. (2009). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Lusekelo, A. (2007). *Tense and Aspects Systems in Kinyakyusa*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Matinde, R.S (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia, Kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Mgullu, R.S. (2010). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Kenya: Longhorn Publishers Ltd.

Ngenzi, M. (2016). *Mfumo wa njeo na nafsi katika vitenzi vya lugha ya Kihehe*. Tasnifu ya Umahiri (haijachapishwa). Chuo kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Nyinondi, O. (2013). *Tense and Aspect in Lugulu*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Rubanza, Y.I. (1996). *Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2019). *Lugha na Sarufi: Kitabu Cha Mwanafunzi Kidato Cha Tano na Sita*. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Wesana-Chomi, E. (2003). *Kozi Tangulizi katika Sarufi Miundo ya Kiswahili*. Sebha: Chuo Kikuu cha Sebha.

Wesana-Chomi, E. (2013). *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.